

C o n t e n t s

• Financial highlights	2
• Letter of transmittal	4
• TemboCARD services network	6
• Chairman’s statement	8
• Review of operations	12
• Financial results	20
• Economic review	22
• Report of the directors	26
• Statement of the directors’ responsibilities	34
• Report of the auditors	36
• Income statement	37
• Balance sheet	38
• Statement of changes in equity	39
• Cash flow	40
• Notes to the financial statements	41
• CRDB Bank addresses	55



Vielelezo vya mwaka ulioishia 31 Disemba 2002

F i n a n c i a l





H i g h l i g h t s

**For the year ended
31st December 2002**

Vielelezo Muhimu vya kifedha

Financial highlights

BILIONI ZA SHILINGI	Tshs. IN BILLIONS				
Maelezo	Particulars	1999	2000	2001	2002
Jumla ya rasilimali	Total assets	130.6	190.4	230.9	303.3
Mikopo	Loans	34.4	34.9	33.8	43.3
Uwekezaji katika dhamana	Investment in debt securities	47.6	68.9	94.0	123.2
Amana	Deposits	108.2	160.7	201.9	269.7
Mtaji	Share capital	8.3	8.3	8.2	8.2
Mali ya wanahisa	Owners equity	12.5	14.1	14.1	15.2
Uwiano muhimu	Key ratios	1999	2000	2001	2002
Pato na rasilimali	Return on assets	0.39	0.87	0.82	0.4
Pato na mali ya wanahisa	Return on equity	3.2	11.7	13.4	7.2
Pato kwa kila hisa moja Tsh.	Earnings per share Tshs	500	2000	2304	1336
Gawio kwa kila hisa moja Tsh.	Dividends per share Tshs.	0	1100	1000	1000



TemboCARD ATM ya Benki ya CRDB



CRDB Bank TemboCARD ATM

Barua ya kuwasilisha

Wapendwa: Wanahisa na Wateja wetu,

Ninayo furaha kuwasilisha kwenu taarifa ya mwaka 2002. Taarifa hii ina hesabu za mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2002, matukio na maendeleo muhimu pamoja na mustakabali wa biashara.

Wenu mwaminifu.



Jerry Solomon

**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
Benki ya CRDB**

Letter of transmittal

Dear: Shareholders and customers,

It is a pleasure to present to you the Bank's Annual Report for the year 2002. The report contains the Annual Accounts, major events, achievements and future business prospects.

Yours Sincerely



Jerry Solomon

**Chairman of the Board of Directors
CRDB Bank**

Dira

Tunataka kuwa benki ya kizalendo inayoongoza na inayopata faida, inayowajali wateja, inayotoa huduma na bidhaa bora na inawapa wanahisa gawio zuri. Tutakuwa na mtandao wa vituo vya huduma kote nchini karibu na wateja, uongozi madhubuti na wafanyakazi wenye ujuzi na waliohamasika kutoa huduma bora.

Azma

Sisi ni benki ya kizalendo inayoongoza, inayotoa huduma bora za kifedha, ikizingatia wateja wadogo na wa kati, na huduma binafsi kwa makampuni makubwa. Sambamba na hayo, tunawahakikishia wanahisa gawio linalolingana na la washindani. Kupitia mtandao ulioenea nchini wa matawi yaliyounganishwa kufanya kazi pamoja, na wafanyakazi waadilifu, wateja wanapata huduma kwa urahisi nchini kote.





Vision

We aspire to be a local leading profitable retail bank, which is customer-need driven with high quality products and services, offering competitive returns to shareholders. We will have wide, fully linked outreach in Tanzania with strong, effective management, competent, professional and motivated staff.

Mission

We are a leading local Tanzanian bank providing quality financial services with a strong focus on retail clients and customized corporate services while ensuring competitive returns to shareholders. Through our wide linked branch network and dedicated staff, we offer convenient access throughout the country.



-  **Matawi ya Benki ya CRDB**
-  **CRDB Bank branches**
-  **Huduma za TemboCARD**
-  **TemboCARD services**

T a a r i f a y a M w e n y e k i t i

Mwaka 2002 ulikuwa na matukio mengi yaliyoihusu Benki. Mwaka huu Benki ilipiga hatua kubwa kwenye huduma za wateja, kwa kuwa benki ya kwanza kuingiza Tanzania 'smart card' ikiwa chini ya chapa yake yenyewe ya TemboCard. Hizi kadi za kufanya malipo bila fedha taslim ndizo za kisasa kabisa katika sekta ya kifedha duniani kote.

Matokeo ya kifedha

Mazao makuu ya biashara yaliendelea kupata bei ndogo katika soko la dunia. Bei za mauzo nje ya nchi ziliendelea kupungua zikilinganishwa na zile za manunuzi kutoka nje ya nchi. Kutokana na haya matukio pamoja na uchumi ambao haukuwa na nguvu, kwa mwaka mwingine tena, mikopo haikutumika kikamilifu. Hata hivyo kutokana na usimamizi mzuri wa mikopo, tengo dhidi ya hasara lilipungua kutoka 8.4% mwaka 2001 mpaka 5.5% mwaka huu.

Benki ilipata faida, kabla ya tukio lisilokuwa la kawaida, ya Tsh. milioni 2,891 ikilinganishwa na Tsh. milioni 2,705 ya mwaka 2001. Hata hivyo kwa kuweka tengo dhidi ya hasara ambayo inaweza ikatokana na wizi wa tawi la Azikiwe, Benki ilipata faida baada ya kodi ya Tsh. milioni 1,063 ikilinganishwa na Tsh. milioni 1,818 ya mwaka 2001. Uwiano kati ya pato na mali ya wanahisa uliteremka kutoka 13.4% mwaka 2001 mpaka 7.2% mwaka 2002. Pato kwa kila hisa moja pia lilipungua kutoka Tsh. 2304 mwaka 2001 mpaka Tsh. 1336 mwaka 2002.

Bodi ya Wakurugenzi imependekeza kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka gawio la Tsh. 1000 kwa kila hisa.

Hali ya Benki kifedha iliimarika ikilinganishwa na ya mwaka uliotangulia kwa kuongezeka kwa jumla ya rasilimali kutoka Tsh. bilioni 230.9 mpaka Tsh. bilioni 303.3, ukuaji wa amana kutoka Tsh. bilioni 201.8 mpaka Tsh. bilioni 269.7 na uwekezaji kwenye dhamana za serikali kutoka Tsh. bilioni 128.9 mpaka Tsh. bilioni 166.5.

Maendeleo

Benki iliongezea nguvu huduma zake za malipo ilipoanzisha Mfumo wa Malipo wa TemboCard. Malipo ya toka zamani yanatumia fedha taslim, hundi ikiwa ni pamoja na za wasafiri, kusafirisha fedha na akaunti za benki za aina mbali mbali. TemboCard ambayo inatumia teknolojia ya mfumo wa kompyuta wa "electronic chip" iliyowekwa kwenye kadi, hutumika kupata huduma za kibenki kwenye vituo vya ATM na pia kulipia bidhaa na huduma kutoka kwa wafanyabiashara wanaoshiriki kwenye Mfumo wa Malipo wa TemboCard. Kuna maendeleo mengine mapya kwenye sekta ya mabanki ambayo Benki itayatathmini ili kuona kama yapo itakayotaka kuyatumia kuboresha huduma za wateja.

Shukurani

Ninashukuru kwa ushirikiano niliopata kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi katika kipindi chote cha taarifa hii. Napenda pia kuushukuru uongozi na wafanyakazi kwa kujituma kufanya kazi na hivyo kuiwezesha Benki kuwa na nafasi nzuri ya kuendelea kuwa na mafanikio mazuri katika hii sekta yenye ushindani mkubwa.

Ninapenda pia kuwashukuru wateja wetu kwa kuendelea kuwa nasi na hivyo kutupa nafasi ya kuwapa huduma.



Jerry Solomon
Mwenyekiti

Chairman's Statement

Year 2002 was a very eventful year for the Bank. It is the year that the Bank set a milestone in its customer services by being the first bank to introduce in Tanzania a smart card under its own TemboCard brand, which is one of the new developments in convenient cashless means of payment in the financial world.

Financial results

Low world market prices for agricultural commodity crops persisted, as did the deterioration in the country's terms of trade. This, coupled with the less than robust economic performance, led to another year of unutilised credit facilities. However due to better credit portfolio management, provisions decreased from 8.4% made in year 2001 to 5.5% of the total loan portfolio this year.

The Bank made a profit of TZS 2,891 million, before provision of an exceptional loss compared with the TZS 2,705 million realised in year 2001. However due to the provision made on the probable loss from the robbery at Azikiwe branch, the Bank recorded a profit of TZS 1,063 million compared to TZS 1,818 million in year 2001. Return on equity as a result of the above, dropped from 13.4% in year 2001 to 7.2% in year 2002. Earnings per share also decreased from TZS 2,304 in year 2001 to TZS 1,336 in year 2002.

The Board has recommended to the Annual General Meeting a dividend of TZS. 1000 per share.

The Bank's financial position was strengthened by the growth of its total assets from TZS 230.9 billion to TZS 303.3 billion, growth of its deposits from TZS 201.8 to TZS 269.7 billion and investments in debt securities and loans from TZS 128.9 billion to TZS 166.5 billion.

Developments

The Bank gave its payments services a major boost with the introduction of the TemboCard Payment System. Traditional payment services are based on cash, cheques including traveller's cheques, transfer of funds and various bank accounts. TemboCard, which is a chip based technology, is a dual debit/ATM card. As a debit card it is used to make payments for goods and services. It is also used to access ATM services. There are other interesting new developments in the financial industry, which have a potential of improving the services that our customers enjoy. These will be evaluated for possible adoption by the Bank to improve customer service.

Acknowledgements

I am thankful for the support I enjoyed from the Board during the entire period covered by this report. I wish to commend management and staff for their dedicated services, which have positioned the bank for continued success in one of the most competitive industries in Tanzania.

I also wish to thank our esteemed customers for their loyalty and for giving us the privilege to serve them.



Jerry Solomon

Chairman.

TemboCARD

Kama fedha taslim... lakini muafaka zaidi.





TemboCARD

Just like cash... but more convenient.

M a p i t i o y a u t e n d a j i

Mwaka 1999 Benki ilikamilisha zoezi la kuweka kompyuta zinazoendesha shughuli za msingi za kibenki zinazoweza wateja wapate huduma. Hili zoezi liliambatana na uunganishwaji wa matawi yote kwenye mtandao ili wakati wowote kompyuta za tawi lolote, ziweze kupata taarifa zilizo kwenye kompyuta za matawi mengine yote na pia zipokee taarifa mara zinapoingia kwenye kompyuta za tawi lolote. Mwaka 2002, Benki ilianza kutumia uwezo unaotokana na maendeleo mapya kwenye sekta ya huduma za kibenki ulimwenguni, kuongeza ubora wa huduma za wateja na pia kuhakikisha kuwa wateja wanapata urahisi zaidi wa kutumia huduma zake za kibenki na wana uhuru wa kuamua njia, mahali na muda wa kupata huduma hizo. Hakuna shaka kwamba uanzishwaji wa Mfumo wa Malipo wa TemboCARD utafuatwa na hatua zingine kama hizi ili kuendelea kumpa mteja wa Benki ya CRDB huduma zilizo rahisi kwake kuzitumia na za kisasa.

Mfumo wa Malipo wa TemboCARD

Novemba 8, 2002 Benki ya CRDB ilianzisha hapa Tanzania Mfumo wa Malipo wa TemboCARD unaotumia teknolojia ya 'smart card'. CRDB ni benki ya kwanza kuleta Tanzania Mfumo wa Malipo wa kisasa kabisa unaotumia teknolojia ya namna hii. Benki inao washirika wengi wafanyabiashara ambao wanapokea malipo ya kadi za TemboCARD kwa kulipia bidhaa au huduma na pia kubadilisha fedha zilizo kwenye kadi kwa fedha taslim. TemboCARD pia hutumika kwenye vituo vya ATM kupata huduma kama vile kupata fedha taslimu, kuulizia salio la akaunti, kupata taarifa fupi ya akaunti na kadhalika. TemboCARD pia hutumika kama kitambulisho cha wateja wa Benki ya CRDB kote kwenye mtandao wake wa matawi.

TemboCARD inatumika kwenye biashara nyingi sana kwenye miji ya Dar es Salaam, Arusha, Moshi, Mwanza, Iringa, Morogoro, Songea, Mbeya na Sumbawanga. Huduma hii itasambazwa kwenye mikoa mingine kabla ya Juni 2003. Bidhaa na huduma za aina nyingi sana zinapatikana kwenye biashara za Washirika wetu. Hizi ni pamoja na vituo vya mafuta, supermarkets, dry cleaners, maduka ya madawa, mahoteli, migahawa, na kadhalika ambayo yapo katikati ya miji pamoja na vitongojini. Toka awali washirika wa benki walikuwa wengi na hivyo kuwapa wateja nafasi kubwa ya kuchagua bidhaa, huduma na mahali pa kuzipata. TemboCARD ilikubalika mapema sana na hata zaidi ya matarajio. Hii iliwawezesha wateja wengi zaidi kunufaika na usalama, urahisi na uwezo wa TemboCARD wa kukidhi mahitaji ya aina kadhaa. Baada ya kuchangamkia simu za mikononi, Watanzania walionyesha tena wepesi wao wa kupokea bidhaa mpya bunifu yenye manufaa makubwa. Muda

mfupi baada ya kuanzishwa, ililazimika kuongeza uwezo wa kutengeneza kadi za TemboCARD kuzidi ule uliokuwepo. Kuhifadhi fedha kwenye TemboCARD ni rahisi. Madirisha mahususi ya kuweka fedha za elektroniki kwenye TemboCARD yametengwa matawini ili kutoa hii huduma kwa haraka bila mteja kulazimika kukaa kwenye foleni za huduma zingine za matawini. Mipango ya kuwawezesha wateja kupata hii huduma kwenye ATM za Benki inakamilishwa.

TemboCARD ina tahadhari nyingi za kiusalama zinazozuia mteja asiibiwe kwa udanganyifu ama kupoteza fedha zake iwapo kadi yake itaibiwa au kupotea. Hata hivyo wateja wanao wajibu wa kutomueleza mtu yeyote yule namba yao binafsi ya utambulisho ambayo ni ya siri. TemboCARD ni muhimu sana katika kupeleka huduma za kibenki huko vijijini kwa bei muafaka.

Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, ndiye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya kuzindua TemboCard iliyofanyika kwenye tawi la Holland House tarehe 8/11/2002.

Mikopo

Mikopo iliongezeka kutoka kiwango cha wastani cha Tsh. bilioni 34 kilochodumu kwa miaka mitatu iliyopita na kufikia Tsh. bilioni 43. Ongezeko hili lilitokana na uwezo mkubwa zaidi wa kusimamia mikopo uliopatikana kutokana na hatua kadhaa zilizochukuliwa kuanzia mwaka 2001. Hatua muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na mafunzo maalum kwa wafanyakazi na utengenezaji wa programu za kompyuta za kushughulikia mikopo pamoja na kurudisha mamlaka ya kutoa maamuzi ya mikopo makao makuu tu. Katika kipindi chote cha mwaka 2002 sekta nyingi za uchumi nchini ziliendelea kuwa hafifu kama mwaka 2001. Mahitaji madogo ya soko yaliyotokana na hali hii yalifanya mikopo iliyokuwa imeidhinishwa kutotumika kikamilifu. Kati ya jumla ya mikopo ya Tsh. bilioni 75 iliyoidhinishwa kufikia tarehe 31 Desemba 2002 ni mikopo ya Tsh. bilioni 44 tu iliyotumika. Mazao yanayouzwa nje ya nchi yaliendelea kupata bei ndogo kwenye soko la dunia. Hii ilipunguza mahitaji ya mikopo ya kuuza mazao nje ya nchi. Pamoja na hali ngumu ya masoko, wafanyabiashara wa mazao ambao ni pamoja na vyama vikuu vya ushirika walimudu kulipa mikopo yao vizuri.

Ubora wa hali ya mikopo uliongezeka kwa kiasi cha kuridhisha. Tenge dhidi ya hasara ya mikopo iliyodorora ilishuka kutoka asilimia 8.4 kwa mwaka 2001 na kufikia asilimia 5.5 mwaka 2002. Mfumo mpya wa kutathimini na kukisia athari za mikopo ulichangia katika uboreshaji wa mikopo.

R e v i e w o f o p e r a t i o n s

In 1999 the Bank completed the automation of its core banking processes as well as linking all its branches so that they operate on-line and on a real time basis. In year 2002 the Bank decisively moved to harness the potential of new developments in the financial services industry to further improve the quality of its customer service as well as ensure that customers enjoy more convenience and freedom on how, where and when they do their banking. The Bank's introduction of TemboCARD Payment System will definitely be followed by similar initiatives so that its customers continue to enjoy easier and more valuable banking.

TemboCARD Payment System

On 8th November 2002 CRDB Bank formally launched TemboCARD electronic payment system in Tanzania. It is the first bank to bring to Tanzania the most advanced payment system based on chip technology that is universally known as Smart card. The Bank has very many merchant partners who operate retail outlets where TemboCARD electronic money is accepted in payment for goods and services as well as offering cash to customers in exchange for electronic money. TemboCARD is a dual card that also gives access to such services as cash withdrawals, balance enquiry, mini statements etc at CRDB Bank's ATMs. In addition TemboCARD is an identity card that is used by the Bank for customer identification throughout its network.

TemboCARD, which is a debit card, is accepted by very many outlets in Dar Es Salaam, Arusha, Moshi, and Mwanza, Iringa, Morogoro, Songea, Mbeya and Sumbawanga. Its rollout to the remaining regions will be completed before June 2003. Our Merchant partners, who offer a very wide range of goods and services, include operators of such outlets as fuel filling stations, supermarkets, dry cleaners, pharmacies, hotels, restaurants and pubs etc located both in business centres and residential suburbs. The pool of merchant partners at the outset was large and therefore gave TemboCARD customers a wide range of choice of products, services and convenient outlets. The high and early acceptance of TemboCARD brought the safety, convenience, and flexibility of TemboCARD to more Tanzanians than was anticipated at the early introductory stage. After the lightning speed with which they embraced mobile phones, Tanzanians demonstrated once again their openness to valuable and innovative products. In fact, shortly after launch, it became necessary to raise TemboCARD issuing capacity above the installed capacity in order to meet the very high demand.

Storing money in TemboCARD is simple. Dedicated TemboCARD service tellers with terminals for loading

electronic money are now available in branches. Access to the service is fast and free of any queuing for other services. Arrangements are being finalised to enable customers to load TemboCARD at the Bank's ATMs.

TemboCARD has many security features, which make it extremely difficult for a customer to be defrauded or sustain financial loss if the card is stolen or lost. Customers have an obligation not to divulge their Personal Identification Numbers to anybody at all. TemboCARD will be extremely valuable in making banking services accessible to the rural areas in a cost-effective manner.

The launch of TemboCARD was officiated by Honourable Frederick Sumaye, the Prime Minister of United Republic of Tanzania on 8/11/2002 at CRDB Bank Holland House Branch.

Credit

The loan portfolio rose to Tshs 43 billion from the average level of Tshs 34 billion of the past 3 years. This increase followed an enhanced credit management capacity gained as a result of several measures that were taken last year. The major measures included intensive credit staff training and the acquisition of supporting software applications for many of the credit administration processes. Throughout this period many economic sectors continued to perform as poorly as in 2001. As a consequence credit facilities were under-utilised due to low demand. Of the Tshs 75 billion gross loan applications approved by 31st December 2002 only Tshs 44 billion was utilised. Export crops continued to suffer from low world market prices and thus limited demand for commodity financing facilities. In spite of these difficult market conditions crop traders, who include co-operative unions, serviced their loans satisfactorily.

The quality of the loan portfolio improved significantly. Provisions made to cover probable losses decreased from the 8.4% made in year 2001 to 5.5% of the total loan portfolio made in year 2002. A new credit appraisal and risk assessment system contributed to this improvement. These improvements are expected to continue in the coming years as the bank continues its credit management improvement programme.

The market for sale of real estate in Tanzania is, with a few high-end niche exceptions, very underdeveloped. This business is unlikely to develop fast without the government creating supportive market conditions. Without thriving real estate trading, most of the country's real estate is effectively "dead capital". This limits financing, including house loans in the country.

Soko la mali isiyohamishika bado ni changa sana hapa Tanzania ukiondoa sehemu ndogo ya soko la bei kubwa. Hii biashara itakua kwa kasi ndogo iwapo serikali haitajenga mazingira mazuri ya soko hili. Bila kushamiri kwa biashara ya kuuza na kununua majengo, mali ya taifa isiyohamishika ni mtaji usioweza kutumika kikamilifu. Hii inapunguza mikopo inayotolewa ikiwa ni pamoja na mikopo ya nyumba.

Bidhaa mpya

Ulipaji Mishahara Kwa Kutumia Programu Maalumu ya Kompyuta

Katika kuendesha shughuli kisasa inakubalika na wengi na pia imedhihirishwa kiutendaji kwamba shughuli za kampuni, kama ulinzi, kulipa mishahara na kadhalika, ambazo sio biashara zake halisi, huwa za ufanisi zaidi na gharama muafaka zikipatikana kutoka kampuni nyingine ambayo hizo ndizo biashara zake. Benki ya CRDB inatoa huduma ambazo ni za haraka sana na usalama wa hali ya juu, za kulipa mishahara ya wafanyakazi ambazo zinakidhi mahitaji ya wafanyakazi na wajiri kwa pamoja. Baada ya mwajiri kutengeneza orodha ya mishahara, mfumo wa kulipa mishahara ambao ni mwepesi kuutumia, kwa sababu za kiusalama huibadilisha orodha isiweze kusomeka (encryption). Pia huwezesha shughuli zote mpaka kuingiza mishahara ndani ya akaunti za benki za wafanyakazi wanaohusika, kufanyika moja kwa moja na kompyuta, ikiwa akaunti ipo kwenye tawi la Benki ya CRDB au benki nyingine. Mfumo huu huweza kushughulikia mishahara katika fedha za Kitanzania au dola za Kimarekani. Benki ina mtandao na matawi 24 nchini yanayoendeshwa kwa mfumo wa mawasiliano ya wakati ule ule kwa hiyo huchukua sekunde chache tu kuingiza mishahara kwenye akaunti za wafanyakazi nchini kote.

Chini ya mpango huu wafanyakazi wanaruhusiwa kufungua akaunti za mishahara bila kutanguliza fedha za kufungulia akaunti. Vile vile salio la akaunti ni Tsh. 2000 tu. Wafanyakazi pia wanahimizwa kuwa na TemboCARD ili waweze kutoa fedha kwenye akaunti zao kwa kutumia ATM

za Benki ya CRDB wakati wowote mchana na usiku mwaka mzima. Kuna huduma za ziada ambazo zinaweza kuongezwa kama sehemu ya huduma hii kama kuweka fedha za elektroniki kwenye kadi ya TemboCARD kwenye ofisi za mwajiri. Fedha za elektroniki zinaweza kutumika kununulia bidhaa na huduma kutoka kwa wafanyabiashara wengi wanaokubali kulipwa kwa TemboCARD na hata kupata fedha taslimu kutoka kwa wafanyabiashara hao ambao wanatambua athari za matumizi ya fedha taslimu. Huu mfumo wa kulipa mishahara unamhakikishia mfanyakazi kwamba mishahara wake atapatwa mapema bila bughudha na inapunguza sana muda wa kazi anaopoteza akifuatilia mishahara. Pamoja na mwajiri kupunguza masaa yanayopotezwa na wafanyakazi kufuatilia mishahara yao, pia hupunguza gharama za kulipa mishahara, bughudha na hatari ya kuibwa fedha za mishahara.

Huduma za kuuza na kusajili hisa

Mwaka 2002 benki ilianzisha huduma za kuongoza shughuli za kupokea fedha za mauzo kutoka kwa umma unaonunua hisa za makampuni yanayotoa mwaliko wa awali kwa umma ununue hisa zake mpya au za zamani. Benki pia inatoa huduma za kusajili hisa ikiwa ni pamoja na kusajili mauzo na manunuzi yote yanayofanyika na kuendesha shughuli za gawio, kutoa hisa za bonasi na kuwapa wanahisa nafasi ya kwanza kununua hisa mpya. Baada ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kuidhinisha kuuzwa hisa kwa umma, Benki ya CRDB kama kiongozi wa shughuli za kupokea mauzo husimamia shughuli zote toka kugawa ilani ya mauzo ya hisa mpaka kutenga idadi ya hisa ambazo kila mwombaji ataweza kununua, kupokea fedha za mauzo pamoja na kutoa ripoti kamili ya shughuli zote ilizosimamia. Benki inafanya shughuli hizi ikishirikiana vizuri na muuzaji hisa, mshauri wake wa masuala ya fedha, benki nyingine zinazoteuliwa kupokea fedha za mauzo pamoja na madalali wa soko la hisa, wanaoshughulikia hayo mauzo.

New products

Automated Salary Payment

In modern management practice it is widely accepted and it has been conclusively demonstrated that, it is more efficient and cost-effective to outsource such non-core company functions as salary payment. CRDB Bank offers very fast and secure automated salary payment services that simultaneously meet the needs of employers and employees. After the employer completes preparing the monthly payroll, the user-friendly system encrypts and automates the handling of the data including crediting the respective employee bank salary account in whatever branch it may be in CRDB Bank or any other bank. The system handles salary payments in Tshs and USA dollars. With a network of 24 countrywide branches that operate on-line and on a real time basis, the system takes just moments to credit respective employee accounts all over the country.

Employees are eligible to operate a special salary account that can be opened without an initial cash deposit and only requires that a minimum balance of two thousand shillings be retained in the salary account. Employees are encouraged to acquire TemboCARD so that they can make withdrawals at the bank's ATMs anytime of day or night all year round. There are other optional services that may be included in the bundle of services, such as loading TemboCARD at employers' premises. Loaded TemboCARD may be used to make purchases from very many retailers who accept TemboCARD in payment of goods and services or obtain cash from selected retailers. This salary payment service assures employees early access to their salaries while drastically cutting down on the inconvenience and working hours lost chasing salaries. The employer drastically cuts down the working hours lost by employees chasing salaries as well as his salary administration costs, inconvenience and risk of robbery for employers who pay in cash.

Share Floatation and Registraship services

In year 2002 the Bank launched Lead Receiver Bank Services for companies that make public offering of new or existing shares. It also offers Share Registration Services that include keeping the share register updated as well as related administration of dividends, bonus and rights issues. After the Capital Markets and Securities Authority (CMSA) approves share floatation, CRDB Bank, if chosen to be the lead receiving bank, may handle the entire process from the distribution of prospectus to the allotment of shares, the

payment of share proceeds together with a full report of the floatation. The Bank works closely with the respective clients, their financial advisers, and other receiving banks and stock exchange brokers appointed to participate in the floatation.

The administration of a share register is best entrusted to specialised professional firms, for actively traded shares in the stock exchange. CRDB Bank professionally handles all aspects of share administration such as processing and paying dividends, bonus/rights issues and of course the core function of updating the Share Register and preparing required management reports.

Customer Service Improvements

Savings Accounts

The Busara Savings Account and Junior Jumbo Account (J.J. Account) can now be operated as U.S dollar denominated savings accounts. Only CRDB Bank shareholders are eligible for Busara Savings Account while only children below 18 years of age are eligible for J.J. Account. Instead of the previously allowed two withdrawals per year, J.J. Account now allows three to match schools' annual three terms.

Improving access

The Bank established a new agency at TPC in Kilimanjaro region. This is part of the Bank's programme of improving access to its services countrywide. This addition to the Bank's network provides a third outlet for customers in Kilimanjaro region. At the same time it increases the number of mini-branches (static agencies) to five from the previous four. CRDB Bank is continuing with the identification of other locations where it can improve customer access to its banking services in cost-effective ways. The Bank's Microfinance programme pilot phase in the four regions of Mbeya, Iringa Morogoro and Dodoma was successfully completed after the Bank established commercially viable ways of making its services accessible to low income micro entrepreneurs. The Bank now plans to rollout the programme to the rest of the country.

Usajili wa hisa zinazonunuliwa na kuuzwa kwenye soko la hisa unastahili kukabidhiwa kwa wataalam ili ufanyike kwa ufanisi. Benki ya CRDB inashughulikia kitaalamu shughuli zote za kusimamia hisa kama kulipa gawio, hisa za bonasi/za haki ya wanahisa waliopo ya kununua hisa mpya na kutunza daftari la kusajili hisa pamoja na kutengeneza ripoti zinazotakiwa na uongozi wa kampuni.

Kuongeza ubora wa huduma za wateja

Akaunti za Akiba

Akaunti za Akiba za Busara na Junior Jumbo (Akaunti ya J.J.) sasa zinaweza kuendeshwa kwa kutumia dola za Kimarekani. Ni Wanahisa wa Benki ya CRDB pekee wanaostahili kuendesha Akaunti ya Busara. Kwa upande wa Akaunti ya J.J. wenye stahili ni watoto wenye umri chini ya miaka 18. Badala ya nafasi mbili kwa mwaka za kuweza kutoa fedha kwenye Akaunti ya J.J. sasa kuna nafasi tatu ili kuendana na mihula mitatu ya shule kwa mwaka.

Upatikanaji huduma

Benki ilianzisha tawi dogo jipya la TPC mkoani Kilimanjaro. Hii ni sehemu ya programu ya Benki ya kufikisha huduma zake karibu na wateja nchini kote. Kutokana na kupanuka huku kwa mtandao wake wa vituo vya huduma, sasa mkoa wa Kilimanjaro una vituo vitatu. Idadi ya matawi madogo imeongezeka kutoka manne ya awali na kufikia matano sasa. Benki inaendelea kuchunguza maeneo mapya ambako itaweza kuboresha upatikanaji wa huduma zake kwa gharama muafaka. Majaribio ya Mradi wa Huduma za Kifedha kwa Wenye Shunguli Ndogo Ndogo (Microfinance) yaliyofanyika mikoa ya Mbeya, Iringa, Morogoro na Dodoma, yalifanikiwa na hivyo kuwawezesha walengwa kupata huduma za kibenki. Benki inaandaa mpango wa kufikisha programu hii kote nchini.

Uboreshaji wa huduma

Pamoja na kuanzisha TemboCard na huduma za ATM, Benki pia iliboresha maeneo mengine ya huduma zake. Kati ya hizo zinazotajika ni kuongeza uwezo wa mfumo wake wa kompyuta ili kuboresha huduma za wateja na upatikanaji wa huduma kwa wakati muafaka. Pia ukarabati wa matawi ya Benki unaoendelea una lengo hilo hilo la kuboresha huduma za wateja. Mwaka 2002 Benki iliyazindua upya matawi ya Lumumba na Arusha baada ya kukamilisha kuyakarabati. Ukarabati wa matawi ya Vijana, Moshi na Mwanza ulikua unakaribia kukamilika na yanategemewa kuzinduliwa kabla ya Juni 2003. Lengo la kuboresha matawi ni kuyabadilisha kutoka hali ya kizamani na kuyafanya ya kisasa yenye kutoa nafasi nzuri kwa wateja, sehemu nyingi zaidi za kutoa huduma, na kuondoa vikwazo kati ya wafanyakazi na wateja. Matawi ya Tower, Holland House, Morogoro, Kahama na Kigoma ni matawi mengine ya kisasa kabisa. Zoezi la kukarabati matawi bado linaendelea.

Msaada kwa Jamii

Mwaka 2002 misaada ya jamii iliyotolewa na Benki ilielekezwa zaidi kwenye kusaidia shughuli za Vijana na elimu. Benki ilitoa fedha za kujenga vyoo vya Shule ya Msingi ya Uhuru Mchanganyiko. Aidha Taasisi za elimu na shughuli za wanafunzi zifuatazo zilipata msaada wa Benki; Muungano wa Masuala ya Kifedha wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DUFA), Shule ya Msingi ya Busamba, Maadhimisho nchini Tanzania ya Wiki ya Kimataifa ya Wanafunzi, Siku ya wazazi ya Shule za St. Florence na Mwalimu Nyerere, Mashindano ya hisabati kwa shule za miji ya Dodoma na Mtwara pamoja na kisima cha Shule ya Sekondari ya Jitegemee. Shughuli zingine zilizohusu vijana na Asasi zao zilikuwa ni pamoja na misaada kwa Muungano wa Netiboli wa Zanzibar, Tamasha la vijana wa Don Bosco, Siku ya Wanawake Kimataifa, Asasi ya Watoto ya Tushirikiane na Michezo ya Shule ya Kimataifa ya Tanganyika.

Service quality improvements

Besides launching TemboCard and the Bank's ATMs, CRDB Bank made many other improvements to its services. Notable among them were the upgrading of its IT system to improve the quality and timeliness of customer service as well as the on-going refurbishment of its branches. In year 2002 the Bank completed the refurbishment and re-launching of Lumumba and Arusha branches. Vijana, Moshi and Mwanza branches are being refurbished and are scheduled to be re-launched in the first part of year 2003. The purpose of the refurbishment exercise is to turn traditional branches into very modern outlets with spacious and friendly banking halls, more service counters, layouts that facilitate easy customer access to services including meeting rooms and greatly reduced barriers between customers and staff. Tower, Holland House, Morogoro, Kahama and Kigoma branches are the other very modern branches. The refurbishment exercise is continuing.

Community support

Youth and education were the focus of the Bank's community support in year 2002. The Bank funded the construction of toilets for Uhuru Mchanganyiko Primary School. The following educational institutions and student activities received financial support from the Bank; Dar es Salaam University Finance Association (DUFA), Busamba Primary School, International Student Week in Tanzania, St. Florence Academy Parents Day, Mwalimu Nyerere Parents Day, Mathematics competition in Mtwara and Dodoma and a water well for Jitegemee secondary school. Other youth related activities and institutions included funding for Zanzibar Netball Association, Don Bosco Youth Festival, International Women Day, Tushirikiane Children and International School of Tanganyika Sports games.

Bidhaa bunifu zenye faida!
Mazungumzo katika mikutano ya matawi ya wanahisa



Innovative Profitable Products!
The talk at branch shareholders meetings

Mashine ya manunuzi ya TemboCARD
Ipo popote unapofanya manunuzi yako



TemboCARD Point of Sale Terminal
A familiar fixture where you shop

Matokeo ya kifedha

Kwa ujumla ufanisi wa Benki kwa mwaka 2002 umeonyeshwa hapa chini.

Maelezo	Particulars	2002Tsh.Blns		2001Tsh.Blns		Ongezeko/Upungufu Increase/Decrease	%
Mapato ya riba	Financial income	13.9	16.1	-2.2	-13.7		
Mapato mengine	Other income	9.7	8.1	1.6	20		
Gharama ya riba	Financial Expenses	3.5	3.4	0.1	2.9		
Gharama ya uendeshaji	Operating Expenses	16.4	15.2	1.2	8.0		
Mapato halisi ya riba	Financial Spread	10.4	12.7	-2.3	-18.1		
Kinga dhidi ya hasara	Provision	0.76	2.9	-2.1	-74.0		
Faida kabla ya kodi	Pre-tax Profit	1.1	2.7	-1.6	59		

Mapato kutokana na riba

Mikopo kwenye vitabu vya Benki, ambayo ni chanzo kikubwa cha mapato ya Benki, ilifikia kiwango cha Tsh. bilioni 43 mwishoni mwa mwaka 2002 ambapo mwaka 2001 mikopo ilikuwa Tsh. bilioni 34.

Mapato ya riba yalishuka kutoka Tsh. 16.1 bilioni mwaka 2001 hadi Tsh. bilioni 13.9 mwaka 2002 ambayo ni sawasawa na kushuka kwa Tsh. bilioni 2.2 au asilimia 13.7.

Mapato Mengine

Mapato mengine yaliongezeka kwa Tsh. bilioni 1.6 ambazo ni sawa na asilimia 20. Mwaka 2002 jumla ya mapato mengine ilikuwa Tsh. bilioni 9.7 ikilinganishwa na Tsh. bilioni 8.1 zilizopatikana mwaka 2001.

Gharama za kulipa riba

Gharama za riba iliyolipwa kwa amana za akiba, hundi na za muda maalumu, ziliongezeka kwa asilimia 2.9 ambayo ni sawasawa na Tsh. bilioni 0.1, kutoka Tsh. bilioni 3.4 mwaka 2001 na kufikia Tsh. bilioni 3.5 mwishoni mwa mwaka 2002.

Gharama za uendeshaji

Jumla ya gharama za uendeshaji kwa mwaka 2002 zilikuwa Tshs.16.4 bilioni na mwaka 2001 zilikuwa Tshs.15.2. Hili ni ongezeko la Tsh. bilioni 1.2 au asilimia 8.

Riba halisi

Riba halisi (riba iliyopokelewa ondoa iliyolipwa) ilipungua kutoka Tsh. 12.7 bilioni za mwaka 2001 mpaka Tsh. 10.4 bilioni za mwaka 2002. Upungufu huu ni wa Tsh. bilion 2.3 au asilimia 18.1.

Tengo dhidi ya hasara

Tengo dhidi ya hasara kutokana na madeni yaliyodorora ilipungua sana kutoka Tsh. 2.9 bilioni za mwaka 2001 mpaka Tsh. 0.76 bilioni baada ya kuondoa marejesho ya madeni yaliyodorora yaliyolipwa mwaka 2002.

Faida kabla ya kodi

Faida kabla ya kodi mwaka 2002 ilikuwa Tsh. bilioni 1.1 ikilinganishwa na Tsh. bilioni 2.7 ya mwaka 2001. Kumekuwapo na kupungua kwa Tsh. bilioni 1.6 au asilimia 59.

Malimbikizo ya Faida

Mwaka 2002, Benki ilikuwa na limbikizo la faida la Tshs 2,604 milioni, na mwaka 2001 lilikuwa Tshs 2,365 milioni.

Financial results

The Bank's performance in year 2002 is shown in the table on page 19

Financial income

The Bank's Loan Portfolio was TZS 43 billions in year 2002 compared to TZS 34 billions in year 2001. Following a general decline of interest rates in the economy financial income decreased by TZS 2.2 billions or 13.7% from TZS 16.1 billions earned in year 2001 to TZS 13.9 earned in year 2002.

Other income

Other income earned in year 2002 was TZS. 9.7 billions, which is TZS 1.6 billions more than the TZS 8.1 billions earned in year 2001 or an increase of 20%. The main items that increased were commissions and exchange gains.

Financial expenses

Although deposits increased significantly, the Bank recorded a relatively low interest expense. Interest expenses paid on Demand deposits, Savings and Time deposits increased from TZS 3.4 billions in year 2001 to TZS 3.5 billions in year 2002. This is an increase of TZS 1 billion or 2.9%.

Operating expenses

Operating expenses, including staff and administrative expenses for year 2001 were TZS 15.2 billions compared to TZS 16.4 billions in year 2002. This is an increase of 1.2 billions or 8%.

Financial Spread

Financial spread decreased by TZS 2.3 billions or 18.1% from TZS 12.7 billions in year 2001 to TZS 10.4 billions in year 2002.

Loan Loss Provisions

Provision for bad and doubtful debts decreased sharply from TZS 2.9 billions in year 2001 to TZS 0.76 billion net of recoveries in year 2002.

Pre-tax Profit

Profit before tax was TZS 1.1 billions in year 2002 compared to TZS 2.7 billions in year 2001, a decrease of Tshs. 1.6 billion or 59%.

Accumulated Profit

The bank had an accumulated profit of TZS 2,604 million in year 2002, whereas in year 2001 the bank had the accumulated profit of TZS 2,365 million.

M a p i t i o y a u c h u m i

Mtizamo wa jumla

Uchumi wa nchi ulikuwa mzuri kwa wastani pamoja na kupungua kwa bei ya bidhaa zinazouzwa nje zikilinganishwa na bei za bidhaa zinazonunuliwa kutoka nje. Pato halisi la Taifa (GDP) lilikua kwa asilimia 6.3, ambayo ni kubwa kuliko asilimia 5.3 ya mwaka 2001. Vielelezo vikuu vya hali ya uchumi vilikuwa imara kwa ujumla. Uchimbaji madini na utalii ndizo sekta zilizoongoza. Uchimbaji madini uliendelea kuongezeka kwa asilimia zaidi ya 13. Kwa upande mwingine kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo iliongezeka kutoka asilimia 3 za mwaka 2001 na kufikia asilimia 7.6 za mwaka 2002. Baadhi ya Vielelezo vya kiuchumi vimeoneshwa hapa chini.

Selected Economic Indicators in percentage terms

Baadhi ya Vielelezo vya uchumi kama asilimia

Vielelezo Indicators	1997	1998	1999	2000	2001	2002
Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa Real GDP Annual Growth	3.3	4.0	4.8	5.1	5.3	6.0
Mfumuko wa bei CPI Inflation (headline) end of period	15.4	11.2	7.0	5.5	4.9	4.4
Wastani wa faida ya dhamana za serikali za muda mfupi Treasury bills weighted average yield	11.4	11.8	15.5	5.5	4.0	4.5
Riba ya mikopo ya muda mfupi Short term lending rate	23.3	22.4	20.4	15.7	14.9	15.0
Riba ya mikopo ya muda wa kati na mrefu Medium and long term lending rate	24.3	22.0	20.1	21.6	17.6	18.0
Riba kwa amana za miezi kumi na miwili Twelve months deposit rate	10.1	11.5	10.2	8.6	5.9	5.7

Biashara ya nje

Mwaka 2002 nakisi katika urari wa biashara ya nchi za nje ilipungua pengo kwa asilimia 20.3 na hivyo kuacha pengo la dola za Kimarekani milioni 589.4 kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya nje na kupungua kwa manunuzi kutoka nje. Mauzo ya nje yalikuwa dola za Kimarekani milioni 1,541 na manunuzi ya nje yalikuwa dola za Kimarekani milioni 2,139.5. Thamani ya mauzo ya nje ya kawaida ilipungua kwa asilimia 12.8 kufuatia kushuka kwa wingi na bei zake. Licha ya chai na tumbaku ambazo wingi wa mauzo yake yaliongezeka, mauzo ya mazao mengine yaliyobaki yalipungua.

Bei ya fedha za kigeni

Thamani ya shilingi ya Tanzania iliendelea kupungua dhidi ya fedha za kigeni zinazotumika sana duniani. Hii ilisababishwa na kupungua kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na bidhaa tunazouza nchi za nje kuwa pungufu kuliko mahitaji ya nchi ya fedha za kigeni, pamoja na mfumuko wa bei nchini Tanzania kuwa juu kuliko kwenye nchi tunazofanya nazo biashara. Fedha za wafadhili ambazo kwa kawaida hupunguza pengo la fedha za kigeni, hazikupatikana kwa kiasi kilichotegemewa. Hii ilizidisha udhaifu wa shilingi ya Tanzania. Kwenye soko la mabanki la fedha za kigeni shilingi ilikuwa na thamani ya wastani wa shilingi za Tanzania 916 kwa dola moja ya Kimarekani mwanzoni mwa mwaka 2002 na kufikia shilingi 985 mwisho wa mwaka. Kuna wakati shilingi iliteremka mpaka kuwa 1000 kwa dola moja. Shilingi ya Tanzania pia ilipungua thamani dhidi ya fedha zingine za kigeni zinazotumika sana duniani.

Mfumuko wa bei

Mfumuko wa bei uliendelea na mwelekeo wake wa kupungua. Kulikuwa na kupungua kutoka asilimia 5.5 ya mwaka 2001 hadi asilimia 4.5 mwaka 2002. Kupungua huku kulihusishwa zaidi na mavuno mazuri ya chakula. Mfumuko wa bei za chakula ulipungua kutoka asilimia 6.1 mwaka 2001 mpaka asilimia 2.9. Mfumuko wa bei za bidhaa zisizo chakula uliongezeka kutoka asilimia 2.5 mwaka 2001 mpaka asilimia 9.0. Kupungua kwa ujumla kwa mfumuko wa bei kunatokana na hali nzuri ya hewa na sera za serikali za mapato na matumizi yake, pamoja na ujazo wa fedha kwenye uchumi.

E c o n o m i c r e v i e w

Overview

The country's economy performed relatively well in year 2002 despite deteriorating terms of trade. Real GDP growth was 6.3 percent, which was a significant improvement over the 5.3 percent attained in the previous year. The macro-economic performance remained generally stable. Mining and tourism were the leading sectors with mining maintaining a growth rate of over 13 percent. On the other hand the agricultural sector's growth accelerated from 3 percent in year 2001 to 7.6 percent in year 2002. Selected macro-economic indicators are summarised in the table on page 21.

Foreign trade

In year 2002, the trade account improved by 20.3 percent to a deficit of USD 598.4 million due to increase in exports coupled with a decrease in imports. Total exports amounted to USD 1,541.1 million against imports of USD 2,139.5 million. Traditional exports declined by 12.8 percent following a decline in both volume and unit prices. Except for tea and tobacco whose volume increased, the volume of all traditional products declined.

Exchange rate

The Tanzanian shilling continued to depreciate against major world currencies. This is attributed to the overvaluation of the Tanzanian shilling against other currencies of major trade partners as a result of general deterioration of the country's foreign exchange receipts from its traditional exports compared to its foreign exchange financing needs coupled with a positive inflation differential. Donor funding which normally reduces the

foreign exchange deficit was not available in the amounts projected and therefore further aggravated the weakness of the Tanzanian shilling. On the inter-bank foreign exchange market, the shilling went from a weighted average rate (WAR) of TZS/USD 916 at the beginning of the year 2002 to 985 at the end of the year. At one point the shilling depreciated to TZS/USA 1,000. The shilling also depreciated against other major currencies.

Inflation

The annual inflation rate continued its downward trend, remarkably declining from the year 2001 rate of 5.5 percent to 4.5 percent. The decline was mainly attributed to the bumper food harvest. Food inflation declined from 6.1 percent in year 2001 to 2.9 percent. Non food inflation increased from 2.5 percent in 2001 to 9.0 percent. The overall decline of inflation is due to both the favourable weather and the government's monetary and fiscal policies.

Lipia mlo wako kwa TemboCARD



Settle your dining bill with TemboCARD

Chukua gawio lako hapa kwa kutumia TemboCARD



Use TemboCARD to collect your dividend here

Taarifa ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia 31 desemba 2002

Wakurugenzi wanawasilisha taarifa yao pamoja na hesabu za mwaka zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2002.

SHUGHULI

Lengo la msingi la Benki ni kuendesha shughuli za Benki ya biashara kwenye matawi yake yote, ikiwa ni pamoja na kupokea amana, kukopesha, biashara za fedha za kigeni na huduma zingine zikiwa ni pamoja na kusafirisha fedha na ununuzi na uuzaji wa dhamana mbalimbali.

MATOKEO

Katika mwaka unaozungumziwa, kabla ya tengo dhidi ya hasara isiyo ya kawaida iliyotokana na wizi wa kutumia nguvu kwenye tawi la Azikiwe, Benki ilipata faida ya Tsh. milioni 2,891 ikilinganishwa na Tsh. milioni 2,705 za mwaka 2001. Hata hivyo baada ya tengo dhidi ya hasara inayoweza kutokana na wizi huo, Benki ilipata faida ya Tsh. milioni 1,063 ikilinganishwa na faida ya Tsh. milioni 1,817 za mwaka 2001.

Tarehe 15 Novemba 2002, wezi wenye silaha waliingia kwenye tawi la Azikiwe na wakaiba fedha zinazolingana na shilingi za Tanzania milioni 3,150. Wakurugenzi wametumia busara na uhafidhina kwa kuweka tengo la shilingi milioni 2,005.

Mwaka 2002 hali ya kifedha ya Benki iliimarika kama inavyoonyeshwa kwa kuongezeka kwa jumla ya rasilimali kutoka shilingi bilioni 230.9 mpaka shilingi bilioni 303.3 na kupanda kwa amana kutoka shilingi bilioni 201.8 mpaka shilingi bilioni 269.7 pamoja na kuwekeza kwenye dhamana za serikali na mikopo kulikoongezeko kutoka shilingi bilioni 128.9 mpaka shilingi bilioni 166.5

MAENDELEO YA BIASHARA

Katika jitihada za kuboresha huduma za wateja na kupanua huduma za kifedha kwa umma kwa jumla, tarehe 8 Novemba 2002, Benki ilianzisha bidhaa ya "Smart Card", ambayo ni mfumo wa malipo wa TemboCard usiotumia fedha taslimu. Fedha za elektronik huhifadhiwa kwenye

"chip" ya kompyuta iliyochimbiwa kwenye kadi ya TemboCard, na huwezesha wateja kulipia bidhaa na huduma kutoka kwa wauzaji mbali mbali na pia hutumika kwenye ATM (mashine zinazojiendesha zenyewe zinazotoa baadhi ya huduma za kibenki). ATM sita zimewekwa kwenye matawi ya Lumumba, Holland House, Azikiwe, Arusha, Moshi na Mwanza. Hadi Desemba 2002 vituo vya biashara 104 vilikuwa na mashine zinazoweza TemboCard kutumika kufanya malipo. Matumizi ya teknolojia hii yamewezesha Benki kupunguza muda ambao mteja anatumia kupata huduma kwenye matawi; yameleta mbadala wa fedha taslimu; yameongeza usalama wa fedha; uwezo wa Benki kuongeza wingi wa bidhaa zake na vianzo vya mapato.

Benki imekuwa ikifanya majaribio ya mpango wa kutoa huduma za kifedha kwa wenye shughuli ndogo ndogo katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa and Mbeya. Malengo muhimu yaliyofikiwa katika awamu hii ya utekelezaji ni pamoja na kupatikana kwa Asasi za kati 37 ambazo ni washirika wa Benki zenye jumla ya wateja 12,180 kulinganisha na 5,321 wa mwaka 2001. Idadi hii ni pamoja na wanachama wanawake ambao ni 30%. Asasi hizi za kati zimeongeza mikopo zinayotoa kwa wanachama wake kutoka Tsh. milioni 785.8 mwaka 2001 mpaka Tsh. bilioni 5.0 ilipofika mwisho wa Desemba 2002. Jumla ya fedha walizokopesha ni pamoja na mikopo waliyopata kutoka Benki ya CRDB ambayo ilikuwa Tsh. milioni 1,880 ikilinganisha na Tsh. milioni 36.5 za mwaka 2001. Ongezeko hili linatokana na uwezo wa Asasi hizi ambao ulitanuka kutokana na Benki kuwapa mafunzo wafanyakazi 44, wajumbe wa kamati 344 na wanachama wa kawaida 4,437. Mafanikio yamekuwa ya kutia moyo na biashara imeonyesha ni ya kuvutia, kwa hivyo imeamuliwa kusambaza programu hii kwenye mikoa mingine kwa kuanzia na Dar es Salaam.

Benki iliendelea kukarabati matawi yake kwa nia ya kuongeza nafasi na ufanisi kwa wateja wanapokuwa matawini na pia kuyapa matawi sura ya chapa ya Benki ya CRDB. Ukarakati wa matawi ya Lumumba na Arusha ulikamilika na hayo matawi kuzinduliwa upya. Ukarakati wa matawi ya Moshi, Mwanza na Vijana ulikua unakaribia kukamilika. Idadi ya matawi yaliyokarabatiwa itaongezeka

Report of the directors for the year ended 31 december 2002

The directors present their report together with the audited financial statements for the year ended 31 December 2002.

ACTIVITIES

The Bank's primary objective is to carry on the business of commercial banking in all its branches including taking deposits, lending, foreign exchange and other banking services including money transfers and securities/bond/trading.

RESULTS

During the year under review, before provision against an exceptional loss resulting from a robbery at the Azikiwe Branch, the Bank recorded profit before exceptional item of Tshs. 2,891 million compared with Tshs. 2,705 million realized in 2001. However, due to the provision made on the loss from the robbery, the Bank recorded a profit for the year of Tshs. 1,063 million against Tshs. 1,817 million in year 2001.

On 15 November 2002 armed robbers entered Azikiwe branch and stole money in local and foreign currency equivalent to Tshs. 3,150 billion. Directors have made prudent and conservative provision of Tshs. 2,005 million.

During the year, the Bank's financial position strengthened as shown by an increase in its total assets from Tshs. 230.9 billion to Tshs. 303.3 billion, deposits from Tshs. 201.8 to Tshs. 269.7 billion and investments in debt securities and loans from Tshs. 128.9 billion to Tshs. 166.5 billion.

DEVELOPMENT OF THE BUSINESS

In a bid to improve customer service and expand financial services to the broad public, the Bank launched a smart card product, TemboCARD payment system, on 8 November 2002 that stores money in a chip and enables customers to buy goods and services from various outlets and use Automatic Teller Machines (ATMs). Six ATMs were installed at Lumumba, Holland, Azikiwe, Arusha, Moshi

and Mwanza branches and 104 Points of Sale distributed to merchants to support the product. The introduction of this technology has enabled the Bank to improve customer turn-around time in banking halls, provide alternative means of cash handling and security, and has increased the Bank's capacity to broaden its products base and sources of income.

